

TAARIFA YA BARAZA LA BIASHARA WILAYA YA MPWAPWA

1.0 UTANGULIZI

1.1 BARAZA LA BIASHARA TAIFA

Baraza la Biashara ni jukwaa la majadiliano na ushauri kati ya sekta binafsi na sekta ya umma. Baraza la Biashara taifa lilianzishwa kwa Waraka wa Rais Na.1 wa mwaka 2001 na kuchapishwa kwenye gazeti la serikali Na.39 la tarehe 28 septemba 2001.

1.2 BARAZA LA BIASHARA MKOA NA WILAYA

Mabaraza ya Biashara ya Mikoa yalizinduliwa tarehe 15 Machi 2005 na Mh. Benjamin Mkapa, Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, awamu ya tatu, wakati wa mkutano wa tatu wa Baraza.

Mabaraza ya Wilaya yalizinduliwa na Rais Mstaafu, Mh. Jakaya M. Kikwete tarehe 4 Desemba 2008, wakati wa Mkutano wa tano wa Baraza uliojadili "Uwekezaji Wananchi Kiuchumi"

1.3 BARAZA LA BIASHARA WILAYA YA MPWAPWA

Baraza la Biashara Wilaya ya Mpwapwa lilizinduliwa rasmi tarehe 20/04/2015 na aliyekuwa mkuu wa mkoa wa Dodoma Mhe Dk. Rehema Nchimbi. Ambapo baraza lina jumla ya wajumbe 40, ishirini (20) kutoka sekta ya umma na ishirini(20) kutoka sekta binafsi.

2.0 MADHUMUNI NA MAJUKUMU YA BARAZA LA BIASHARA

Dhumuni kuu ni kuwakutanisha Sekta Binafsi na Serikali ili kujadili na kupeana ushauri wa namna ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika Wilaya kwa ajili ya kukuza uchumi. Majukumu mengine ni pamoja na

- Kutengeneza mazingira bora ya kufanyia Biashara na uwekezaji.
- Kuibua fursa za uwekezaji
- Kuzinadi fursa hizo-kupitia kongano mbalimbali.

3.0 MAFANIKIO YA BARAZA LA BIASHARA WILAYA YA MPWAPWA TANGU KUENZISHWA KWAKE

- Baraza la Biashara limewezesha kufanyika kwa marekebisho ya sheria ndogo za Halmashauri
- Ufahamu juu ya tozo mbalimbali toka mamlaka ya chakula, dawa na vipodozi(TFDA)
- Makubaliano juu ya ulipwaji wa ushuru kati ya ushuru wa nyumba za kulala wageni (hotel levy) na ushuru wa huduma (service levy).
- Matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika kukusanya mapato ya ndani.
- Baraza limeweza kuibua na kuwezesha ujenzi wa kituo cha huduma za Biashara (one stop business center).

- Mahusiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma yameboreka ukilinganisha na awali kabla ya Baraza la Biashara kuwepo.

4.0 CHANGAMOTO

1. Wajumbe wengi wa baraza la Biashara kutumia jukwaa hili la majadiliano, kama sehemu ya siasa na kubishana na serikali badala ya kujadili ajenda za kujenga na kuleta maendeleo.

5.0 VIKAO VYA BARAZA LA BIASHARA

Vikao vya Baraza la Biashara vipo kisheria na vipo katika kalenda ya Halmashauri ya Wilaya, hivyo kalenda hiyo inapaswa kufuatwa na kuheshimiwa. (*Taarifa ya vikao vilivyofanyika kwa kipindi cha mwaka 2015-January 2018 imeambatanishwa katika kiambatanisho A.*)

6.0 HITIMISHO

Kutokana na mafanikio tuliyoyaona hapo juu, ambayo yamepatikana kutokana na uwepo wa baraza la Biashara ni wazi kuwa chombo hiki ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Wilaya ya Mpwapwa katika Nyanja za Biashara na uwekezaji, hivyo basi kama tulivyoanza kushirikiana leo tudumishe ushirikiano wetu ili kukifanya chombo hiki kilete mafanikio zaidi.